

afisa ugani au mtaalamu wowote aliye karibu nawe.

- Piga dawa kama vile *Karate* ikiwa mbaazi imeshambuliwa na wadudu wanaonyonya majani na wanaotoboa mifuko.

Kuvuna

- Vuna mahindi yako wakati masuke yamekauka.
- Kata matawi ya mbaazi zilizokauka.

Usindikaji na matumizi

- Pukuchua na pepeta mahindi yako mahali pasafi kama vile sakafu au turubali.
- Anika mahindi vizuri kabla ya kuyahifadhi kupunguza magonjwa ya kutu au fangasi.
- Pigapiga mbaazi kuondoa kwenye mifuko.
- Pepeta mbaazi ili kuondoa uchafu.
- Anika halafu weka dawa za kuhifadhi mahindi na mbaazi kama vile *Actellic Super*.
- Hifadhi kwenye vihenge, magunia au madramu.



Kipeperushi hiki kimetayarishwa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo, Selian, kilichopo Arusha, Tanzania. Kimefadhiliwa na muungano wa kuleta mapinduzi ya kijani Afrika (AGRA) na washirika wengine kama taasisi ya kuendeleza utafiti wa mazao katika kanda kame za tropiki (ICRISAT) na jukwaa la afya ya udongo (ASHC). Inapatikana pia kwenye wavuti wa mradi (www.sari-shp.org) na ASHC (www.cabi.org/ashc).



Kwa taarifa zaidi, wasiliana na afisa ugani au Mkurugenzi wa Kanda ya Kaskazini au Meneja wa mradi (Stephen Lyimo)
Selian Agricultural Research Institute (SARI),
Sanduku La Posta: 6024, Arusha
Simu: +255 73 6500538/80 / +255 754 380 115
Barua pepe: selian.tz@gmail.com au sdnlyimo@yahoo.com

Kufanya kazi kwa pamoja na wadai/wabia kutayarisha taarifa zinazohusu mbuni husishi za afya ya udongo

Ongeza mavuno na kipato

kilimo mseto cha mahindi na mbaazi



Taasisi ya utafiti na maendeleo na kilimo kanda ya Kaskazini

Mbaazi ni zao la biashara, linaongeza rutuba na ni chanzo cha protini kwa kaya. Unaweza kupanda mbaazi yenyewe au ukachanganya na mazao mengine kama vile mahindi, mtama, viazi vitamu na mihogo.

Kilimo mseto cha mahindi na mbaazi kinaongeza rutuba ardhini. Pia unaweza kuongeza mavuno na kipato chako mara mbili kama ukitumia mbolea zenye kiritubisho cha fosforasi wakati wa kupanda.

Mbegu za mbaazi

Muda wa kukomaa	Idadi ya siku hadi kukomaa	Alna ya mbaazi	Mavuno (magunia ya kilo 100 kwa ekari)
Muda wa kati	140-180	Tumia, ICEAP 00554, ICEAP 00557	8-10
Muda mrefu	180-270	Mali, ICEAP 00053, ICEAP 00932, ICEAP 00936, ICEAP 576-1	10-12

Chagua aina ya mahindi yanayofaa kwa kilimo mseto katika eneo lako.

Kutayarisha shamba

- Lima kwa kutumia trekta au maksai mara tu baada ya kuvuna ili kuchanganya masalia ya mazao kwenye udongo.
- Lima mara ya pili mwezi mmoja kabla ya mvua kunyesha ili kuwezesha magugu yaliyoota kuoza kabla ya kupanda. Piga haro ili kutayarisha shamba vizuri.

Kupanda

- Weka mistari kwa nafasi ya sm 60.
- Weka nafasi ya sm 50 kati ya mashimo kwenye mistari.
- Chimba shimo kina cha sm 5-6.



- Panda mstari mmoja wa mahindi ukifuatiwa na mstari wa mbaazi.
- Panda mahindi na mbaazi wakati mmoja baada ya mvua za kwanza.

Uwekaji wa mbolea za kupandia

- Weka mbolea ya Minjingu Mazao au Minjingu *Phosphate Rock* chengachenga au DAP (tazama jedwali). Kama unatumia mbolea samadi, mahitaji ni viganja viwili vya mbolea kwenye shimo (4–6 tani kwa ekari).
- Weka udongo kiasi baada ya kuweka mbolea. Kisha weka mbegu mbili za mahindi kwenye mistari ya mahindi na mbegu mbili za mbaazi kwenye mistari ya mbaazi. Funika mbegu kwa udongo.
 - Mbegu inaweza kuungua na isiweze kuota ikigusana na mbolea.

Viwango vya mbolea za kupandia

Aina ya mbolea za fosforasi	Idadi ya mifuko ya kina ya kilo 50		Idadi ya vifuniko vya soda vilivyojaa kwa shimo
	kwa hektari	kwa ekari	
Minjingu Mazao	5	2	1½
Minjingu chengachenga (Minjingu <i>Phosphate Rock</i>)	3	1¼	1
Di-Ammonium Phosphate (DAP)	2	¾	½

ANGALIZO:

- Mbolea ya samadi Iliyooza na kuhifadhiwa vizuri inaweza kuchanganywa na za viwandani kuongeza mavuno.

Palizi na kuweka mbolea ya kukuzia kwenye mahindi

- Fanya palizi ya kwanza wiki mbili baada ya mbegu za mahindi kuota.
- Punguza miche ubakize miwili kwa shimo.
- Palizi ya pili ifanywe wiki 5-6 baada ya mahindi kuota.
- Baada ya palizi ya pili, wakati udongo una unyevu wa kutosha, weka kifuniko kimoja na nusu (1½) cha urea au mbolea nyingine ya kukuzia karibu na shina la mahindi. Hakikisha umefunika mbolea yako mara baada ya kuweka.

Wadudu waharibifu na magonjwa ya mbaazi

- Panda mbaazi ambazo zina ukinzani wa ugonjwa wa *Fusaria mnyauko*.
- Ng'oa na kuchoma mimea iliyoshambuliwa na ugonjwa wa *Fusaria mnyauko*.
- Tumia nafasi sahihi ya kupandia kupunguza uwezekano wa ugonjwa wa *Fusaria mnyauko*.
- Pia zingatia kilimo cha mzunguko mazao kwenye mashamba yaliyoathirika na ugonjwa wa *Fusaria mnyauko* kama vile alizeti na mihogo.
- Kwa kawaida, wadudu waharibifu wa mbaazi wanashambulia majani, maua na mifuko. Kama mashambulizi yakiwa makubwa tafuta mashauri kutoka kwa